
## TAHADHARI

- Usitumie dawa moja mara kwa mara ili kuepuka usugu wa fangasi.
- Fanya uchunguzi wa mara kwa mara ili kubaini ugonjwa mapema.
- Hakikisha hakuna mabaki ya mazao yanayooza kwenye shamba.

### Muhimu/Hitimisho

DOA JEUSI ni tishio kwa uzalishaji wa machungwa lakini linaweza kudhibitiwa kwa kuzingatia usafi wa shamba, matumizi sahihi ya dawa, na ufuatiliaji wa karibu wa afya ya mimea.



Madhara ya Doa Jeusi
(Black Spot)

TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES AUTHORITY


## Wasiliana nasi:

080 011 003 1

dg@tphpa.go.tz

www.tphpa.go.tz


## Scan for More


@tphpa_tz

TPHPA TV

P.O. Box 3024 , Arusha - Tanzania
Nairobi Rd, Ngaramtoni Area


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA KILIMO**

**MAMLAKA YA AFYA YA MIMEA NA VIUATILIFU TANZANIA**



# DOA JEUSI (BLACK SPOT)

## UTAMBUZI

Ugonjwa wa machungwa unaosababishwa na fangasi
Ugonjwa huu huathiri sana machungwa ya kibiashara, hasa katika maeneo yenye mvua nyingi na unyevunyevu wa mara kwa mara.

### 1. DALILI KUU

- Madoa madogo meusi kwenye maganda ya matunda.
- Doa huweza kuzungukwa na duara la njano.
- Matunda huanza kuoza taratibu.
- Majani pia yanaweza kuonesha madoa ya hudhurungi au meusi.
- Matunda yanaweza kudhoofika na kudondoka kabla ya kuiva

### 2. MADHARA KWENYE MACHUNGWA

- **Upotevu wa mavuno:** Matunda yaliyoathirika hayawezi kuuzwa sokoni.
- **Kupungua kwa ubora wa matunda:** Hata kama hayaozi kabisa, sura ya nje huharibika.
- **Kudhoofika kwa mti:** Ikiwa ugonjwa umeenea, huathiri uwezo wa mmea kutoa matunda bora msimu unaofuata.
- **Kupoteza soko la kimataifa:** Wateja wa nje hukataa matunda yenye doa jeusi

## UDHIBITI WA DOA JEUSI (BLACK SPOT)

### a) Njia za Kibiolojia

- Tumia viuatilifu vya kiasili vya fangasi (Trichoderma spp)ambayo ni rafiki anayepambana na fangasi wa doa jeusi.

### b) Njia za Kiikolojia/Kilimo Bora

- Ondoa na teketeza majani na matunda yaliyoathirika.
- Punguza msongamano wa miti shambani ili kupunguza unyevu
- Limia kwenye udongo wenye mzunguko mzuri wa hewa na maji.

### Matumizi ya Viuatilifu.

- Tumia viuatilifu vya ukungu(fungicides) mfano Copper Sulfate Pentahydrate 2 1.46%), Mancozeb
- Piga dawa kila baada ya wiki 2-3 wakati wa msimu wa mvua



Doa Jeusi (Black Spot) Kwenye Chungwa